

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI

KIKAO CHA PILI

01 FEBRUARI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI

KIKAO CHA PILI – TAREHE 01 FEBRUARI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

20. MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (UKONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itawalipa mafao waliokuwa Wafanyakazi wa Viwanda vya Kilitex na Sunguratesh Gongolamboto.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

21. MHESHIMIWA MUSUKUMA JOSEPH KASHEKU (GEITA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya kutoka Kata ya Katoma kwenda Nyambaya utaanza.

22. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO (MIKUMI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya kuunganisha Ruaha Mbuyuni, Malolo hadi Uleling'ombe.

23. MHESHIMIWA DAIMU IDDI MPAKATE (TUNDURU KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupandisha Shule za Sekondari za Mchoteka na Nalasi kuwa za Kidato cha Tano na Sita Wilayani Tunduru.

24. MHESHIMIWA JOSEPH ANANIA TADAYO (MWANGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka sharti Vikundi vya Wanawake na Vijana kuwa na Mtu mwenye Ulemavu kwa mikopo ya Halmashauri.

25. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga soko la Tengeru kwa kiwango cha Kimataifa.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

26. MHESHIMIWA JUDITH SALVIO KAPINGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, kuna mkakati gani wa kurekebisha Sheria ili ubakaji na ulawiti kwa Watoto uwe na kifungu tofauti cha Sheria.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

27. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Vituo vya Polisi vya Tarafa ya Mang'ula na Kidatu vitakarabatiwa.

28. MHESHIMIWA MWATUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma za kipolisi jirani na maeneo ya Wananchi.

WIZARA YA NISHATI:

29. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuondoa kero ya ukatikaji wa umeme nchini hasa katika maeneo ya biashara kama Kariakoo.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

30. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALEKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini mnara wa mawasiliano ya simu utajengwa Kata ya Mamba Kusini Jimbo la Vunjo.

31. MHESHIMIWA JOHN MARKO SALLU (HANDENI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini minara ya simu itajengwa katika maeneo ambayo hayana mawasiliano katika Jimbo la Handeni Vijijini.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

32. MHESHIMIWA JESCA JONATHAN MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mkakati gani wa kutochelewesha vibali vya kuruhusu umeme kupita kwenye hifadhi za misitu ili kuwahisha usambazaji umeme Vijijini.

33. MHESHIMIWA GODWIN EMMANUEL KUNAMBI (MLIMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini mgogoro wa mipaka kati ya Vijiji vya Utengule, Ovindembo, Ipinde, Tanganyika na Kampuni ya Kilombero *North's* utatatuliwa.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

34. MHESHIMIWA HAMIDA MOHAMED ABDALLAH (LINDI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kusaidia ujenzi wa Chuo Kikuu cha Uvuvi na Usafiri Baharini Lindi.

WIZARA YA AFYA:

35. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itaboresha kadi ya kliniki ya Watoto chini ya miaka mitano ili kusaidia ufuatiliaji wa wingi wa damu.

36. MHESHIMIWA MARGARETH SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

- Je, ni lini Serikali itabadilisha Sera ya Chanjo kitaifa ili kuwakinga watu wengi zaidi badala ya kutibu mtu aliye na ugonjwa tayari.

IV. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA BIASHARA NA MAZINGIRA:

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**DODOMA
01 FEBRUARI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

